

JINA LA MWANAFUNZI
S/SEKONDARI.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBAGHAI
KOROGWE- TANGA

Mkuu wa shule ya sekondari mbaghai anayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari mbaghai kwa mwaka wa masomo 2021. HONGERA na KARIBU sana mbaghai sekondari.

Muhula wa masomo utanza tarehe **11/01/2021**. Hivyo unatakiwa kuripoti shuleni tarehe na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2021**

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

a) SARE YA SHULE

Mzazi/mlezi hakikisha mototo wako anaripoti akiwa na sare sahihi ya shule

MVULANA

- i. Suruali za rangi nyeusi (**black**) mfano wa kitambaa umeambatanishwa kwenye fomu hii MODAL HAZIRUHUSIWI.
- ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi
- iii. Viatu vyeusi kamba na soksi nyeupe

WASICHANA

- i. Sketi mbili ndefu zinazogusa kisigino zenye rinda boksi na belti ya kawaida, rangi ya kitambaa ni kijani cheusi (**dark green**) mfano wa kitambaa umeambatanishwa kwenye fomu hii
- ii. Nusu kazu nyeupe na hijabu inayofunika mikono kwa wasichana waislam na mashati mawili meupe kwa wasichana wakristo
- iii. Viatu vyeusi vyenye kamba na soksi nyeupe.

NB

- Bajaji, kandambili na yeboyebo haviruhusiwi
- Sketi ya kijani ambayo haiendani na rangi iliyoambatanishwa kwenye fomu hii haitakubaliwa

VIFAA VYA DARASANI

- i. Madaftari makubwa (**counter book 12**)
- ii. Kalamu za wino wa bluu au nyeusi
- iii. Mkebe (**mathematical set**)
- iv. Begi la kubebea madaftari (**mifuko ya Rambo hairuhuiwi**) rula na penseli
- v. Rim moja (**A4**)

VIFAA VYA KUFANYIA USAFI

- i. Ndoo ndogo, jembe, fyekeo/kwanja na fagio la chelewa

VIFAA VYA MICHEZO

- ii. Track suit rangi ya kijani
- iii. Raba na soksi

NB: Vifaa vya kufanyia usafi na michezo vitakaguliwa siku ya kuripoti

KARIBUNI SANA MBAGHAI SEKONDARI

.....
DISMAS M. MBOYA
MKUU WA SHULE